HISTORIA FUPI YA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA – DAYOSISI YA KUSINI

Ujio wa wamisionari ukanda wa kusini mwa Tanzania

Msafara wa wamisionari wa Kijerumani wa chama cha Misioni cha Berlin (pia Berlin I) kutoka Afrika Kusini kilifika mahali palipoitwa Wangemanshore, katika nchi ya Wanyakyusa, ncha ya kaskazini ya Ziwa Nyasa tarehe 25 September 1891 na kujenga mahema hapo. Wamisionari hawa walikuja kwa wito / ombi la chifu wa Unyakyusa Mwakatungila. Jina la asili la mahali hapo walipofikia ni Pipagika. Ila wamisionari walipaita Wangemanshore kwa jina la Rais wa chama cha Misioni cha Berlini. Wamisionari hawa walikaribishwa hapo na chifu wa Wanyakyusa aliyeitwa Mwakatungila.

Chama cha Misioni cha Berlin kilianzishwa mwaka 1824 na Wakristo wa kiuamsho waliokuwa na moto wa kupeleka Injili kote duniani. Hapa Afrika walikuwa tayari wameanzisha misioni katika nchi ya Afrika Kusini.

Msafara huo uliongozwa na Misionari Alexander Meresky na ulikuwa na watu 10, wazungu 8 na Waafrika 2. Majina ya wazungu wengine ni Carl Nauhaus, ambaye Waafrika walimwita “Kyamba”, Christian Schumann au “Mwakikato”, Bunk au “Buungu”, and Franke. Franke aliugua na kurudi Afrika Kusini na kufariki mwaka 1892. Wazungu wengine watatu ambao walikuwa ni mafundi wa majengo walikuwa ni: Rohring, Krause na Th. Nauhaus. Wawili wengine walikuwa ni Waafrika wa Kizulu walioitwa Afrika na Nathanael.

Kwa sababu mbalimbali, mwaka 1899 stasheni ya misioni ya Pipagika ilihamishiwa Itete, ndani ya Unyakyusa yenyewe. Kutoka hapo wamisinari walitawanyika na kuanzisha stesheni za misioni katika maeneo mbalimbali: Manow mwaka 1892, Mwakaleli 1893, Ikombe 1893 (ilihamishiwa Matema mwaka 1909). Huko Ukinga misioni zilijengwa Bulongwa 1895 na Tandala 1897.

Katika eneo la Ubena / Uhehe stesheni zilianzishwa Kidugala mwaka 1898, Mufindi 1898, Emmaberg 1898, Lupembe 1899, Muhanga 1899 (ilihamishiwa Pomern

mwaka 1912), Yakobi 1899, Ilembula 1890. Huko Uwanji stesheni ilijengwa Magoye mwaka 1900, Upangwa ilijengwa Milo mwaka 1902 na Usangu ilianzishwa Brandt mwaka 1908. Hatimaye, mwaka 1913 stesheni za misioni zilianzishwa katika maeneo ya Wambungu na Wamasagati huko Lwamate and Kingori.

Kidugala



Katika Ubena wamisionari walifika baada ya kukaribishwa na Chifu Ngera (Ngela), akitarajia kupata msaada wa kivita dhidi ya Chifu Merere wa kabila la Wasangu aliyevamia eneo la Ubena kutoka Magharibi. Hivyo, wamisionari Christoph Bunk, Willhelm Neuberg, Martin Priebusch na Paul Gröschel walifika Kidugala tarehe 13 July 1898. Wenyeji waliwapenda wamisionari kwa sababu waliwasaidia kuwaondoa maadui zao na kutibu magonjwa, hususani ugonjwa wa ndui.

Kidugala ilikuwa ni makao makuu ya Kanisa la Kilutheri la Tanganyika ya Kusini hadi mwaka 1963 ambapo makao makuu yalihamishiwa mjini Njombe. Kutoka Kidugala kazi ya Injili ilifanyika sehemu nyingi ya ukanda wa kusini. Maeneo ambayo Injili ilifika ni pamoja na yale ambayo leo ni maeneo ya kiutawala ya mikoa ya Njombe, Mbeya, Iringa, Morogoro, Mtwara na Lindi. Baadhi ya maeneo hayo sasa yamekuwa ni dayosisi zinazojitegemea. Dayosisi hizo ni Dayosisi ya Kusini Kati, Dayosisi ya Iringa, Dayosisi ya Ulanga – Kilombero, Dayosisi ya Konde, Dayosisi ya Mtwara na Dayosisi ya Ruvuma.

Madhara ya vita na uongozi wa kanisa

Wachungaji wa kwanza nane wa Kiafrika wa Kanisa la Kilutheri Tanganyika Kusini waliobarikiwa tarehe 05 Mei, 1934 kanisani Lupembe, Njombe wakiwa na Wamisionari wa Kijerumani. 1. Herman Wilhelm Neuberg 2. Ludzabiko Havanga Nyato 3. Lutangilo Melele 4. Alatuvanga Msitu 5. Ananidze Chungu 6. Mkuu wa Kanisa, Julius Oelke 7. Yohana Nyagava 8. Mtendzi Kyelula 9. Josefu Mpogolo 10. Ludzabiko Kihupi 11. Mkuu wa Shule Kidugala, Mchg. Klaus.
Chanzo: Nyaraka kuukuu, Maktaba iliyoko Seminari ya Kilutheri Kidugala, tarehe 26 Aprili, 2019.

Kazi ya Injili iliathiriwa na Vita ya Maji Maji (1905 – 1907), Vita ya Kwanza na ya Pili ya Dunia (1914 – 1918 na 1939 – 1945). Wakati wa vita kuu za dunia miundo mbinu mingi ya kanisa iliharibiwa na wamisionari wa Kijerumani waliondolewa na kurudishwa kwao. Kanisa likabaki ukiwa.

Hata hivyo, ilikuwa ni wakati huo wa ukiwa, ndipo wakristo wenyeji walipochukua wajibu wa kuliongoza Kanisa. Hivyo, tarehe 5 Mei 1934 wachungaji nane walibarikiwa Lupembe, ambapo mojawa wao, Yohana Nyagava (namba saba katika picha), alichaguliwa kuwa Rais wa Kanisa Desemba 1939. Hata hivyo, mchungaji huyu aliongoza kwa muda mfupi tu, maana aliondolewa na badala yake akawekwa Mchg. Martin Nordfeldt kutoka Swedeni. Waswedeni waliongoza kanisa kuanzia mwaka 1941 hadi 1959. Nyagawa aliondolewa kwa tuhuma na ushawishi kadhaa dhidi yake. Hili halikuwa jambo lisilotegemewa, maana kipindi hicho watawala wa serikali ya kikoloni na wamisionari walikuwa

wanahusiana na kutegemeana. Mahusiano haya yasingeruhusu hali ya kujitambua kwa wenyeji.

Mwaka 1963 Kanisa la Kilutheri la Tanganyika ya Kusini liliungana na makanisa mengine sita ya Tanganyika kuunda kanisa moja, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanganyika (KKKT). Makanisa saba yaliyounda KKKT ni:

- Kanisa la Kilutheri Tanganyika ya Kusini lenye Rais kama Mkuu wa Sinodi.
- Kanisa la Kilutheri Tanganyika ya Kaskazini lenye Askofu kama Mkuu wa Dayosisi.
- Kanisa la KiInjili la Buhaya linaloongozwa na Askofu kama Mkuu wa Dayosisi
- Kanisa la Kilutheri la Usambara/Digo lenye Rais kama Mkuu wa Sinodi.
- Kanisa la Kilutheri la Tanganyika ya Kati lenye Rais wa Sinodi
- Kanisa la Kilutheri la Iraq lenye Rais wa Sinodi.
- Kanisa la Kilutheri la Uzaramo – Uluguru lenye Rais kama Mkuu wa Sinodi.

Muungano huu wa makanisa saba ulifanyika Azania Front, Dar es Salaam (Makao Makuu ya KKKT) tarehe 19 Juni 1963, na maadhimisho yake ya miaka 50 (1963 – 2013) yalifanyika Chuo Kikuu cha Tuamini Makumira tarehe 23 Juni 2013.

Sinodi ya Kusini ilikuja kuwa Dayosisi tarehe 27 Septemba 1981, ambapo Mchg. Dkt. Yuda Bernard Matata Kiwovele alisimikwa kuwa askofu wa kwanza. Kwa mfuatano hadi leo, Dayosisi imeongozwa na maaskofu wafuatao:

- Askofu Dkt. Yuda Bernard Matata Kiwovele (1981 – 1987)
- Askofu Lunogelo Mwanalufunga Vuhahula (1987 – 1991)
- Askofu Zephania Andefidze Mgeyekwa (1991– 2003)
- Askofu Cleopa Akutulaga Lukilo (2004–2011)
- Askofu Isaya Japhet Mengele 2011–2019
- Askofu Dkt. George Mark Fihavango (2019 hadi leo)

Huduma ya Kanisa: Uinjilishaji, Afya na Shule

Mawodi ya zahanati ya Ilembula, kwa sasa ndio Hospitali ya Kilutheri Ilembula Dayosisi ya KUsini. Picha hii ni kutoka kitabu kilichoandikwa mwaka 1948. Idara ya Nyaraka Kaukuu, KKKT-DKu

Tangu ujio wa Injili katika eneo hili la Kusini mwa Tanzania, Kanisa limefahamika kwa kumhudumia mtu wote; kiroho, kimwili na kiakili kwa njia ya kuhubiri Injili, huduma ya afya na shule.

Kwa upande wa huduma ya kiroho, hadi mwaka 2021 idadi ya Wakristo ni takribani 185,000 na wachungaji 190, ambapo kati yao, 42 hivi ni wastaafu. Idadi ya Majimbo ni saba, sharika 85 na mitaa 591.

Kuhusu huduma ya afya; Dayosisi ina hospitali moja ya Ilembula (hapo mwanzo majengo yake yalikuwa ni kuta za udongo na paa kuezekwa kwa nyasi kama inavyoonekana kwenye picha), kituo kimoja cha Afya cha Kidugala na zahanati

kumi na tatu. Zahanati hizo ni Kidegembye, Brandt, Nyanyembe, Ikuna, Igongolo, Mapanda, Kangaga, Madundasi, Usuka, Yakobi, Ulembwe na Ukalawa.

Kwa upande wa elimu, Dayosisi ina shule za sekondari nne. Kati ya hizo, moja ni mojawapo ya fani za Seminari ya Kidugala. Shule nyingine, ambazo zote ni za wasichana, ni Igumbilo, Emmaberg na Mufindi. Aidha shule nyingine moja itaanza hivi karibuni katika Jimbo la Njombe. Shule zote za msingi, takribani 30 zilitaifishwa na serikali miaka ya 1970. Hata hivyo, Dayosisi hivi karibuni imeanza kuendesha shule moja ya msingi ya mchepuo wa lugha ya Kiingereza. Shule hii iko Nyekamtwe, Njombe.
Aidha, Dayosisi inaendesha vyuo vya kati ambavyo vinatoa certificate na diploma katika theologia na muziki wa kanisa (kwa wainjilisti, wachungaji na wanamziki – Kidugala), Utaalamu ya Tehama, Usimamizi wa Biashara, Maendeleo ya Jamii (katika Chuo cha Amani kilichopo Njombe), Afya na Sayansi Shirikishi (Ilembula) na Ufundi (Mafinga). Malengo ya Dayosisi ni kuzifanya hizi taasisi kuunda chuo kikuu cha Dayosisi.

Uhusiano wa Dayosisi ya Kusini na Makanisa mengine

- Dayosisi inahusiana na vyama vilivyoleta Injili na makanisa kama ndugu na washirika.
- Dayosisi ya Kusini ni sehemu ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).
- Dayosisi ni mwanachama wa muungano wa Kilutheri wa kutoa huduma (LMC) na Shirikisho la Makanisa ya Kilutheri Duniani (LWF).
- Dayosisi ya Kusini hushirikiana na madhehebu mengine katika shughuli za kijamii na maombi, kwa mfano, Siku ya maombi ya dunia.

xxxxxx